- Hifadhi karanga mahali pakavu pasipo na joto.
- Hakikisha karanga zilizohifadhiwa haziozi.
- Kama yanapatikana , tumia dawa ya kibayolojia kamavile Aflasafe™ kwa kufuata ushauri wa wataalam.




*Kudhibiti sumu kuvu kwa kutumia Aflasafe*

## 7. JINSI YA KUVUNA NA KUHIFADHI

- Vuna karanga wakati zimekomaa. Kuvuna karanga kabla ya kukomaa vizuri kunasababisha kupoteza mavuno na kuchelewa kuvuna kunasababisha karanga kuingiwa na sumu kuvu.
- Vuna wakati ambao hakuna unyevu shambani, kisha anika au ondoa vitumba kwanza kwenye miche ya karanga.
- Hifadhi karanga zilizokauka vizuri kwenye magunia safi na ghala safi pasipo na unyevu.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**


1. Mkurugenzi wa Kanda, Utafiti na Maendeleo Kanda ya Kati, Kituo cha utafiti wa Kilimo, Makutupora, S.L.P 1676, Dodoma.

2. Afisa Kilimo na Umwagiliaji, Halmashauri ya Wilaya Kongwa, S.L.P 57, Kongwa.



Kimetayarishwa na ;

Kituo cha utafiti wa Kilimo Makutupora S.L.P 1676, kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Ukanda wa Tropiki (IITA), S.L.P. 34441, Dar Es Salaama, Kupitia mradi wa N2Africa




# Ongeza mavuno ya karanga kwa kutumia mbinu bora za kilimo



IITA
Transforming African Agriculture

# KILIMO BORA CHA KARANGA

## 1. UTANGULIZI

- Karanga ni zao lenye viini lishe vya protini na mafuta kwa wingi. Mabaki ya mimea ya karanga pia yana viini lishe vya protini, hivyo ni chakula kizuri cha mifugo.
- Karanga pia huboresha rutuba ya udongo kwa kuongeza kiasili cha naitrojeni kwenye udongo. Sifa hizi zinafanya karanga kuwa mmea bora katika kilimo cha kuchanganya au kuzungusha mazao hasa jamii ya nafaka.

## 2. AINA BORA ZA KARANGA NA SIFA ZAKE

**Pendo :** Inasimama, inakomaa ndani ya siku 90; mbegu yake ni nyeupe yenye ukubwa wa kadri, inauwezo wa kuzaa hadi kilo 800 za karanga iliyomenywa kwa ekari.

**Mnanje :** Inatambaa, inakomaa ndani ya siku 120, mbegu yake ni nyekundu, kubwa, inauwezo wa kuzaa kilo 850 za karanga iliyomenywa kwa ekari.

**Mangaka :** Inatambaa, inakomaa ndani ya siku 120, mbegu yake ni nyekundu, kubwa, inauwezo wa kuzaa kilo 900 za karanga iliyomenywa kwa ekari.

## 3. JINSI YA KUPANDA

- Karanga huota na kuzaa vizuri kwenye udongo tifutifu wenye rutuba ya kutosha. Panda karanga kwa mistari wakati udongo una unyevu wa kutosha ili kutumia kiwango sahihi cha mbegu, Kurahisisha kuweka mbolea na kupalilia, pia kupata urahisi wa kuvuna.
- Kwaaina zinazotambaa, panda kwa nafasi ya sm 50 mstari hadi mstari, kwa sm 15 mmea hadi mmea .
- Kwaaina zinasimama, panda nafasi ya sm 50 mstari hadi mstari, kwa sms 10 mmea hadi mmea.
- Mbegu zipandwe katika kina cha sentimita 5.

Tumia mbolea ya kupandia aina ya **DAP** na karanga zikianza kutoa maua ongeza mbolea aina ya **Gypsum** kuwezesha mbegu kujaa vizuri katika ganda. Mbolea hizi zitumike katika viwango vinavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini.

| Aina ya mbolea | Kiasi kwa ekari | Kiasi kwa shimo |
|---|---|---|
| DAP | Kilo 50 | Kizobo cha soda kila baada ya futi 2 |
| Gypsum | Kilo 50 | Kizobo cha soda kila baada ya futi 2 |

## 4. PALIZI

Kwa matokeo mazuri, palilia karanga wiki 2 - baada ya kupanda kisha wiki 2 baadaye kutegemea uotaji wa magugu.

## 5. KUZUIA WADUDU

- Zuia wadudu waharibifu kwa kupulizia dawa utakazo shauriwa na mtaalamu wa kilimo.
- Karanga hushambuliwa na wadudu waaina nyingi ila wadudu mafuta ni hatari zaidi. Wadudu hawa huambukiza ugonjwa wa makoko *(Rosette)* na huharibu mimea kwa kuitoboa. Wakitokea pulizia dawa ya Karate 5EC ili kuwaua. Mimea iliyougua ing'olewe na kuifukiwa ardhini.

Ugonjwa wa *"Rosette"* unaweza kudhibitiwa kwa kupanda mbegu zenye ukinzani kama vile Mangaka.



*Wadudu mafuta katika mmea wa karanga*

## 6. KUDHIBITI SUMU KUVU

Ili kupunguza uwezekano wa karanga kuathiriwa na sumu kuvu, kagua na ondoa karanga zilizooza.